**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA RORYA**

**BUGIRE SEKONDARI,**

**S. L. P 250,**

**RORYA – TARIME.**

**MZAZI/MLEZI WA ………………………………………………………………………..**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BUGIRE KIDATO CHA KWANZA 2024**

Ninayofuraha kukujulisha kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii kwa mwaka 2024. Hivyo natumia fursa hii kukupongeza wewe na mwanao. Shule ya Bugire sekondari inapatikana katika Halmashauri ya wilaya Rorya tarafa ya **Girango**, kata ya **Ikoma** katika kijiji cha **Ikoma** umbali wa **Km 43** kaskazini mwa Halmashauri ya wilaya ya Rorya

Masomo yanayofundishwa katika shule hii ni tisa (9) ambayo ni Kiingereza, Civics, History, Kiswahili, Geography, Basic Mathematics, Physics, Chemistry, na Biology.

Masomo yote yanafundishwa Kwa lugha ya Kiingereza (English) isipokuwa somo la Kiswahili.

Mwanao anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 08/01/2024 kwa ajili ya usajili tayari kwa kuanza masomo kwa muhula wa kwanza na mwisho wa kuripoti ni tarehe 22/01/2024.

Mara upatapo fomu hii na kuisoma kwa makini tafadhali unatakiwa kumpatia mwanao mahitaji yote stahiki yaliyoorodheshwa ili kumwezesha kuripoti mapema shuleni bila kupoteza muda wa masoma.

## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 1. SARE ZA SHULE

Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni akiwa na ;-

**A) Wasichana**

- ✓ Sketi mbili (2) moja ikiwa ya rangi ya **Kijani kibichi** iliyoiva sana (**Dark green**) na ya pili ikiwa ya rangi ya **Bluu nyeusi** iliyoiva sana (**Dark blue**) zenye marinda makubwa mbele na nyuma na marinda madogo madogo manne, ziwe na urefu hadi kwenye kifundo cha mguu.
- ✓ Soksi nyeupe jozi mbili (2)
- ✓ Tai mbili (2) muundo wa kipepeo zenye rangi ya kitambaa cha sketi atakazoshona.

**B**) **Wavulana**

- ✓ Suruali mbili (2) moja ikiwa ya rangi ya **Kijani kibichi** iliyoiva sana (**Dark green**) na ya pili ikiwa ya rangi ya **Bluu nyeusi** iliyoiva sana (**Dark blue**) ziwe na marinda matatu na mkunjo kwa chini (Turn up) na upana wa chini ya mguu uwe inchi 16, isiwe ya kubana na kuonesha maungo ya mwili, kwa ushauri kitambaa kitumike cha daraja la kwanza ( **Grade one)** ili kuepuka kuzeeka haraka.
- ✓ Tai mbili (2) ndefu pana zenye rangi ya kitambaa atakachoshonea suruali.
- ✓ Mkanda mweusi utakaovaliwa kwenye suruali zote mbili.
- ✓ Soksi nyeusi jozi mbili (2)

**C) Jinsia zote**

- ✓ Mashati mawili (2) meupe yenye mikono mirefu.
- ✓ Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba vya ngozi jozi mbili (2) visivyo na visigino virefu wala muundo wa buti (**boot**)
- ✓ T-shirt ya rangi ya zambarau iliyoiva sana yenye kola nyeupe na nembo ya shule.
- ✓ Raba za michezo.
- ✓ Truck suit Dark blue itayowekewa nembo shuleni kwa gharama yako na kuvaliwa siku ya michezo.
- ✓ Sweta litakalovaliwa kipindi cha baridi litategemeana na rangi ya sketi Au suruali itayovaliwa.

**C) VIFAA VINGINEVYO**

- Daftari kubwa kumi (10) Counter books Quire 2 au zaidi.
- Vitabu vya masomo yote kama kuna uwezekano
- kamusi ya kiingereza kwa Kiswahili
- kamusi ya Kiswahili sanifu
- Rimu moja (1) Double A kwa mwaka
- Mathematical sets
- Kalamu ya wino wa blue Au Mweusi
- Penseli( HB) na ufutio
- Unashauriwa kumnunulia mwanao vitabu viwili (20) kati ya vifutavyo kwa ajili kujifunzi
    - Mabala The Farmer
    - Hawa The Bus Driver
    - The Magic Garden
    - Kalulu The Hare

**D) CHAKULA CHA MCHANA**

Ni muhimu Kwa wanafunzi kupata mlo wa mchana ili kuongeza ufanisi wa mwanafunzi kitaaluma. Hivyo kamati ya wazazi imependekeza michango ya chakula kama ifuatavyo;

1. Mahindi kasuku (Gorogoro) kumi na mbili (12) kwa nusu muhula au kasuku ishirini nne (24) nusu mwaka.
2. Shilingi elfu sita kwa ajili ya malipo ya mpishi muhula

**E) VIFAA VYA USAFI**

a) Wavulana waje na jembe moja jipya lenye mpini.
b) Wasichana waje na fyekeo moja na ndoo moja ya lita kumi.

**N:B**

- Maelekezo ya zaida yatatolewa siku utakayoripoti na mwanao shuleni.
- Siku ya kuripoti njoo na hii fomu

**2. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

Shule ya sekondari Bugire inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 kama ilivyorekebishwa kwa sharia Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na Sayansi na Teknologia, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais –Tamesemi yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na atapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Maudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kuwahi kwa kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa .
(d) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(e) Kuvaa sare husika kikamilifu ya shule wakati wowote.
(f) Kutunza mali ya umma.
(g) Kuzingatia Ratiba ya shule.
(h) Ni lugha ya kiingereza tu inayotumika kwa mawasiliano uwapo shuleni.

**3. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

(i) Wizi

(ii) Usherati, ubakaji na ushoga

(iii) Ulevi na matumizi ya dawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, mirungi, kubeli na n.k

(iv) Kupigana au kupiga

(v) Makosa ya jinai

(vi) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

(vii) Kuoa au kuolewa

(viii) Kupata mimba , kutoa mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya shule

(ix) Kudharau alama za taifa mfano bendera na wimbo wa taifa

(x) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule na watu.

(xi) Kukataa adhabu kwa makusudi

(xii) Kwenda nje ya mpaka wa shule bila ruhusa wakati wa masomo

(xiii) Kuwa na simu ya mkononi au kiashiria chochote cha simu

(xiv) Kucheza kamari

(xv) Kuingia kwenye kumbi za starehe mfano Bar, nyumba ya kulala wageni (Gesti), vibanda vya kurushia nyimbo , Disko na n.k

(xvi) Utoro

Karibu Sana

……………………………………..

**PHILIMINI S. PHILEMON**

**MKUU WA SHULE**

**SHULE YA SEKONDARI BUGIRE**

**A. FOMU YA MAELEKEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

**1.** JINA KAMILI LA MWANAFUNZI…………………………………………………..

**2.** TAREHE YA KUZALIWA………………………………………………………….

**3.** MZAZI/ MLEZI………………………………………………….............................

**4.** UHUSIANO NA MLEZI…………………………………………………………..

**5.** MAHALI ANAPOISHI MZAZI/ MLEZI…………………………………………........

**6.** NAMBA SIMU YA MZAZI /MLEZI INAYOPATIKANA…………………………….

**7.** KABILA…………………………………. 8. DINI……………………………………..

**9.** KAZI YA MZAZI /MLEZI…………………………………………………………..

**10.** WAZAZI WAKO HAI AU WAMEFARIKI ( Weka alama ya V)

**.** BABA AMEFARIKI (            )       **.** BABA YUPO HAI (       )

**.**MAMA AMEFARIKI (            **)**       **.** MAMA YUPO HAI (       )

**11.** NDUGU WENGINE WA KARIBU NA MZAZI/MLEZI AMBAO WANAWEZA KUTUMIKA KAMA WALEZI WA MWANAFUNZI KAMA MZAZI/ MLEZI HUSIKA HAYUPO

**(a)**……………………………..…………….MAHALI………………NA.SIMU…………………#….

**(b)** ……………………………………..….MAHALI…………………NA.SIMU…………………

**(c)** ……………………………………..….MAHALI…………………NA.SIMU…………………

**(d)** …………………………………….MAHALI……………………NA.SIMU…………………

**B. MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA JINAI**

Mimi (jina la mwanafunzi)………………………………………………………..

Nimesoma na kuelewa sheria, kanuni na utaratibu za shule na nipo tayari kuzitekeleza kwa muda wote nitakapokuwepo shuleni kama mwanafunzi. Nitakapo kiuka au kwenda kinyume na kipengele chochote cha shule adhabu stahiki ichukuliwe dhidi yangu kwa mujibu wa sheria na utaratibu.

Saini ya mwanafunzi………………………… saini ya mkuu wa shule…………………………………

**C. FOMU YA MZAZI/MLEZI KUKUBALINA NA SHERIA, KANUNI, MAELEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE**

Mimi…………………………………………………………………………….……………

Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi……………………………………….…………………………

Nimesoma na kuelewa sheria, kanuni na utaratibu za shule na nimekubaliana nazo kama mzazi wa mwanafunzi na nipo tayari kuzitekeleza sheria hizo pamoja na maelezo yatakayotolewa na shule.

…………………………………………………..

Saini ya mzazi / mlezi wa mwanafunzi

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**PRESIDENT'S OFFICE – REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**BUGIRE SECONDARY STUDENT'S FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

Student's full name.......................................................................................................................................

Age .......................................

I kindly request you to examine him/her physically and mentally if he/she is fit or unfit to pursue O-level studies in our school.

Blood-count ..............................................................................................................................

Urine ..........................................................................................................................................

Stool ...........................................................................................................................................

Venereal – diseases .....................................................................................................................

T. B ............................................................................................................................................

Ears ............................................................................................................................................

Eyes ............................................................................................................................................

Spleen .........................................................................................................................................

Chest ..........................................................................................................................................

**ADDITIONAL INFORMATION:**

If any E.g, physical defects (arm or leg impairments, chronic or family diseases) ect

.............................................................................................................................................................................
.............................................................................................................................................

I certify that he/she is fit/unfit to persue education as stated

Name ........................................................................................................................

Signature ....................................... Station .......................................................

Designation ....................................

Date ................................................ Official stamp.............................................